



**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA**

TAARIFA KWA UMMA

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 15 APRIL, 2020

Wizara ya Afya Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya sita (6) wa Corona (COVID – 19) nchini na kufikia idadi ya wagonjwa 18 kutoka 12 ambao tuliowatolea taarifa tarehe 13 Aprili, 2020.

Taarifa za wagonjwa wapya ni kama ifuatavyo:-

1. Mwanamme, Mtanzania mwenye umri wa miaka 37, mkaazi wa Fuoni.
2. Mwanamme Mtanzania mwenye umri wa miaka 45 mkaazi wa Pangawe.
3. Mwanamme Mtanzania mwenye umri wa miaka 63 mkaazi wa Kijichi aliefariki nyumbani tarehe 11 Aprili, 2020 na kuzikwa siku hiyohiyo.
4. Mwanamme mwenye umri wa miaka 60 mkaazi wa kwamchina.
5. Mwanamke Mtanzania mwenye umri wa miaka 48 mkaazi wa Migombani.
6. Mwanamme Raia wa Egypt (Misri) mwenye umri wa miaka 33 ameingia nchini tarehe 15 Machi, 2020 akitokea Egypt kupitia Dubai kwa Shirika landege la Fly Dubai.


Wagonjwa wote ambao ni Raia wa Tanzania hawana historia ya kusafiri nje ya nchi siku za hivi karibuni.

Wagonjwa wote wamelazwa katika vituo maalum kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuhairisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima.

Aidha Wizara inaomba wananchi ambao wana dadili za homa kali. Kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya Afya na kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huo.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID – 19 kutoka Wizara ya Afya na sip engine popote.


Hamad Rashid Mohammed (MBM)(MBLW),
Waziri wa Afya - Zanzibar.